**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**ILIYOKETI DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA ANUAI NA. 213 YA 2022**

*(Inatokana na Mgogoro wa Kazi Na. CMA/DSM/KIN/266/2022 katika Tume ya Usuluhishi Dar es Salaam, Kinondoni)*

**KATI YA**

**HUSSEIN MUNGI.........................................................1 MLETA MAOMBI**

**ACKY CHARLES..........................................................2 MLETA MAOMBI**

**DANIEL MAKUNDI........................................................3 MLETA MAOMBI**

**NELSON AINEA MKUMBILI.............................................4 MLETA MAOMBI**

**CLEMENT M. MASELE...................................................5 MLETA MAOMBI**

**CLEOPA SWAI............................................................6 MLETA MAOMBI**

**ANISET MIDALA..........................................................7 MLETA MAOMBI**

**DAMACENT MICHAEL....................................................8 MLETA MAOMBI**

**JONATHAN JOAS KABWOTO...........................................9 MLETA MAOMBI**

**EXPERY SHIO............................................................10 MLETA MAOMBI**

**MOSES MAGANGA......................................................11 MLETA MAOMBI**

**IBRAHIM SARUMBO....................................................12 MLETA MAOMBI**

**JOHN MAKASI..........................................................13 MLETA MAOMBI**

**MEXON M. KAMUNTU..................................................14 MLETA MAOMBI**

**FREDY NDELE MALELE................................................15 MLETA MAOMBI**

**JUMA KHAMIS MACHAKI..............................................16 MLETA MAOMBI**

**JOSEPH MEENA........................................................17 MLETA MAOMBI**

**PETRO MPANDA.......................................................18 MLETA MAOMBI**

**UMDATI MGHEM.......................................................19 MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**MILE SOLUTION CO. LTD.............................................1 MJIBU MAOMBI**

**SIGMAX CO. LTD......................................................2 MJIBU MAOMBI**

LabourCourt.Tz.

**UAMUZI MDOGO**

**K. T. R. MTEULE, J.**

**30th June 2022 & 06th July 2022**

Chini ya hati ya dharura, waleta maombi wamewasilisha maombi katika Mahakama hii wakiomba nafuu zifuatazo:-

1. Kwamba Mahakama hii Tukufu iwe radhi kutoa amri ya zuio la muda dhidi ya mlalamikiwa wa kwanza na wa pili au kampuni tanzu zake kutohamisha, kutenganisha, kuzichukua mali tajwa kutoka mikononi mwa waombaji, kuuza au kuondoa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mali zifuatazo ambazo ni Magari, Pikipiki, Splicing Machine pamoja na Laptop, Magari Nos. T 286 DTQ NISSAN X-TRAIL, MC 599 CCS TVS 125, T 854 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, T 227 DTL NISSAN XTRAIL, MC 714 BFH, T 852 DHW NISSAN PICK UP SINGLE CABIN, T 826 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, MC 403 BFK, T 846 DHW NISSAN PICK UP SINGLE CABIN, T 840 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, MC 703 BFH, T 846 DHQ NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, SPLICING MACHINE 5 na LAPTOP 8 hadi uamuzi wa mwisho wa suala linalosubiriwa kuamuliwa mbele ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Na. CMA/DSM/KIN/266/2022.

2. Kwamba Mahakama hii Tukufu iwe radhi kutoa amri kwa walalamikiwa wa kwanza na wa pili kutoa dhamana mbele ya Mahakama hii sawa na kiasi cha mgogoro, ambazo ni jumla ya

Shilingi za Kitanzania **455,298,247/=** au mali yoyote sawa au zaidi ya thamani hiyo.

3. Kwamba Mahakama hii tukufu iwe radhi kutoa amri kuwa mali hizo, magari namba za usajili T 286 DTQ NISSAN X TRAIL, MC 599 CCS TVS 125, T 854 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, T 227 DTL NISSAN XTRAIL. MC 714 BFH, T 852 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, T 826 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, MC 403 BFK, T 846 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, T 840 DHW NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, MC 703 BFH, T 846 DHQ NISSAN PICKUP SINGLE CABIN, SPLICING MACHINE 5 na LAPTOP 8 hadi hapo itakapotolewa uamuzi kamili wa mwisho katika mgogoro namba CMA/DSM/KIN/266/2022.
4. Kwamba Mahakama hii Tukufu iwe radhi kutoa amri za kumzuia mlalamikiwa wa kwanza na wa pili kuendelea kuwapokonya mali hizo toka kwa waleta maombi hadi pale shauri litakapoamuliwa katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA).
5. Gharama za maombi haya.
6. Nafuu nyingine yoyote ambayo Mahakama hii tukufu itaona inafaa kuutoa.

Maombi yaliambatana na hati ya kiapo cha waleta maombi kilichoeleza kisa cha madai yao yaliyofunguliwa Tume ya Usuluhishi kuwadai wajibu maombi mishahara, likizo na michango ya hifadhi ya jamii huku wakidai ukiukaji wa makubaliano ya kimkataba. Kiapo kimeeleza pia

kuwa waleta maombi wamekabidhiwa vifaa tajwa kama vitendea kazi ambavyo vipo chini ya uangalizi wa waleta maombi. Waleta maombi wameomba mali hizo ziendelee kukaa kwao badala ya kuuzwa na wajibu maombi kama walivyoanza kufanya. Waleta maombi wameeleza pia kuwa wamepokea barua pepe ya wajibu maombi kuwataka warejeshe mali zote za kampuni zilizopo mikononi mwao.

Maombi yalisikilizwa kwa mdomo, ambapo waleta maombi waliwakilishwa na Wakili Mussa Daffa na Mwakilishi Binafsi Pascal Temba. Wajibu maombi waliwakilishwa na Wakili Heri Zuku.

Wakili Mussa Daffa, baada ya kuomba kiapo cha waleta maombi kiwe sehemu ya maelezo yake, alirejea kesi ya **Atilio dhidi ya Mbowe 1969, HCD, 284** pamoja na kesi ya **T. Kaare Vs. General Manager, Mara Cooperative Union 1987 TLR 17** ambazo zina mwongozo wa kuzingatia katika kuruhusu maombi ya zuio la muda. Alisema kesi zote mbili ziliweka vigezo vitatu (3) vya kuzingatia ili Mahakama itoe amri ya zuio kwa muda. Vigezo hivyo ni:-

1) Kuwepo na kesi ya msingi inayohitaji kuamuliwa ambayo mleta maombi ana nafasi kubwa ya kushinda.

2) Kuwa kuna hasara kubwa inayoweza kujitokeza.

3) Katika mizania, mleta maombi ataumia zaidi kama maombi yatakataliwa kuliko mjibu maombi kama maombi yatakubaliwa.

Akianza na kigezo cha kwanza, Wakili Daffa alieleza kuwa kwa mujibu wa kiapo cha waleta maombi aya ya 7 kuwepo kwa mgogoro wa kikazi wenye namba CMA/DSM/KIN/226/2022 kunahalalisha kigezo cha kwanza kwani mishahara na likizo ni kitu cha msingi katika mikataba ya kazi. Alisema kuwa kuna madai hayo basi Mahakama hii ione kwamba kuna kesi ya msingi ya kuamuliwa. Alitahadharisha kuwa siyo jukumu la mleta maombi kuingia ndani kujadili uamuzi wa kesi ya msingi.

Kuhusu kigezo cha pili kinachozungumzia hasara kubwa anayoweza kupata mlalamikaji, Wakili Daffa alisema kuwa walalamikiwa wameanza kuuza baadhi ya mali zao ambazo kimsingi ndio mali zinazofahamika kwa walalamikaji na zipo kwenye mikono ya walalamikaji wakizitumia kufanyia kazi. Alitaja mojawapo ya mali hizo kuwa ni magari ambayo wajibu maombi wana kadi zake za umiliki, na kusema ni rahisi kuziuza au kufanya uhamisho (transfer). Ni rai ya Wakili Daffa kwamba walalamikaji watapata hasara kubwa endapo kesi ya Tume ya Usuluhishi itawapa ushindi waleta maombi mali hizi zikiwa zimeshauzwa kwani hawatakuwa na chochote cha kukazia tuzo.

Kuhusu kigezo cha tatu, Wakili Daffa aliwasilisha hoja kuwa waleta maombi wako katika hatari kubwa zaidi ya hasara kubwa kama maombi haya yatakataliwa ikilinganishwa na hasara watakayopata wajibu maombi kama maombi haya yatakubaliwa. Ana maoni kwamba, ikiwa maombi yatakubaliwa, mali zilizotajwa zitaendelea kuwa salama, ila kama yatakataliwa, wajibu maombi wakaruhusiwa

labourcourt.tz

kuendelea kuziuza au kuzihamisha, waleta maombi hawatakuwa na mali yeyote watakayotumia kukaza hukumu. Aliendelea kueleza, kinyume chake ikiwa maombi yatakubaliwa na waleta maombi wakashindwa katika kesi ya msingi, wajibu maombi wataendelea kuwa wamiliki wa mali zao.

Wakili Daffa alirejea maamuzi ya Mahakama hii katika kesi ya **Alex Lazaro Mjoge na wengine 104 Vs. Fastjet Airline Ltd. & mwenzake, Misc. Appl. No. 205 ya 2019** na kueleza kuwa katika mazingira kama haya Mahakama iliwazuia wajibu maombi kuuza au kuhamisha mali. Aliomba maombi yaruhusiwe na Mahakama itoe amri kuwa mali zisiuzwe hadi Tume iamue kesi ya msingi.

Mwakilishi Binafsi Pascal Temba, aliongeza kuwa uwezekano wa waleta maombi kushinda katika shauli lililopo Tume ya Usuluhishi ni mkubwa kutokana na uwepo wa mishahara ambayo haijalipwa kwa waleta maombi.

Katika majibu yake, Wakili Heri Zuku, aliyemwakilisha Mjibu maombi namba 2 aliomba kiapo kinzani kipokelewe kama sehemu ya shauri wasilisho lake. Alikubaliana na wasilisho la Wakili Daffa kuhusu vigezo vitatu vilivyoainishwa na ili kuruhusu ombi la zuio la muda. Kwa maoni yake, vigezo hivyo vinatakiwa viwepo vyote kwa pamoja. Alirejea kesi ya **Abdi Sale Vs. Asac Care Unit Limited na wengine, Land Case No. 71 of 2011** uk. 9, ambapo Mhe. Jaji Muruke alisema vigezo hivi lazima viwepo vyote kwa pamoja. Ni maoni ya Wakili Zuku kuwa si vigezo vyote vimekidhi matakwa ya sheria.



LabourCourt.tz

Akianza na kigezo cha kwanza, alieleza kuwa haitoshi kusema kuna kesi Baraza la Usuluhishi bali waleta maombi walitakiwa waonyeshe kesi hiyo inahusiana vipi na mali wanayoiombea zuio.

Alisema kiapo cha waleta maombi hakina mahali popote kinanpoonyesha uhalali wa waleta maombi kukaa na mali za wajibu maombi kwani madai yao hayajathibitishwa na Mahakama yoyote. Aliwasilisha hoja kuwa Mahakama hii haiwezi kutoa nafuu ya zuio kwa waleta maombi ambao wameamua kukaa na mali bila idhini ya mwenye mali. Alirejea **Kielelezo S2** ambacho ni barua pepe inayoeleza zaidi kitendo cha waleta maombi kukaa na mali ya mjibu maombi bila idhini, aliwasilisha kuwa huu mgogoro unatengenezwa na waleta maombi bila sababu maana hakuna kesi ya msingi CMA.

Kuhusu kigezo cha pili, Wakili Zuku alisema kuwa hakuna hasara yoyote ambayo waleta maombi wanaweza kupata kwa Mahakama hii kukataa ombi la zuio kwani hakuna uthibitisho wowote katika kiapo kuonyesha kuwa mjibu maombi Na. 2 ameanza kuuza mali. Kwa maoni yake, kigezo hakijaonyesha kama waleta maombi watapata hasara yoyote kama maombi yao hayataruhusiwa. Mpaka sasa mjibu maombi anapata hasara kwa waleta maombi kuendelea kushikilia mali zake bila idhini yake.

Kuhusu kigezo cha tatu, Wakili Zuku aiwasilisha hoja kuwa, kwa vile waleta maombi wameshikilia mali za wajibu maombi bila idhini ya mwenye mali, basi hawawezi kuapta hasara endapo maombi yao yatakataliwa. Alitoa hoja kuwa pia wajibu maombi hawajaieleza

Mahakama kama watashinda kesi fidia ya fedha haitakuwa stahiki halali kwao.

Alipinga uhusika wa kesi ya **Fastjet** katika shauri hili akisema kuwa kesi hii ina utofauti na kesi iliyoko mbele ya Mahakama. Alisema kwenye kesi ya Fastjet mali zilikuwa chini ya usimamizi wa mjibu maombi wakati katika shauri hili waleta maombi wanaomba zuio kwenye mali wanayoishikilia wenyewe kinyume na taratibu.

Mwisho Wakili Zuku alitoa hoja kuwa kwa vile wajibu maombi ni kampuni halali ya kitanzania inayomilikiwa na watanzania kama iliyvoainishwa katika kielelezo cha kiapo kinzani - S 4, endapo kutatokea tuzo itakayowataka wajibu maombi walipe waleta maombi, mjibu maombi ana nguvu ya fedha na kampuni inaendelea na biashara. Wakili Zuku alimalizia kwa kuomba kuwa kwa vile vigezo vyote vitatu havijakidhi, maombi yatupiliwe mbali.

Mawakili wa wajibu maombi walifanya majumuisho ambayo pia yatazingatiwa katika uamuzi huu.

Kutokana na mawasilisho ya wadaawa, Mahakama inaona kuwa kuna hoja moja ya kujibiwa katika maombi haya. Hoja hiyo ni **kama waleta maombi wameweza kutoa sababu za msingi za kuishawishi Mahakama kuruhusu ombi la zuio la muda**.

Suala la zuio la muda limetolewa maelekezo katika sheria hukumu nyingi katika Mahakama zetu miongoni mwa hizo zikiwa ni kesi zifuatazo:- **Atilio vs. Mbowe [1969] HCD 284; Suryakant D.**

**Ramji vs. Savings and Finance Ltd. & 3 Others, High Court Commercial Division, Dar Es Salaam, Civil Case No. 30 of 2000 (Unreported); E. AS Industries Ltd. Vs. Trufood Limited [1972] Ea. 420; Giella vs. Cassman Brown [1973] E.A 358; Colgate Palmolive Company Vs. Zakaria Provisional Stores & 3 Others, High Court, Dar Es Salaam, Civil Case No. 1 of 1997; na CPC International Inc. Vs. Zainabu Grain Millers Ltd., Civil Appeal No. 49 of 1999 [CA].**

Kimsingi, vigezo vilivyozungumzwa katika kesi hizi ni vile vitatu vilivyoongelewa na wadaawa katika maombi haya ambavyo ni:-

1) Kuwepo na kesi ya msingi inayohitaji kuamuliwa ambayo mleta maombi ana nafas kubwa ya kushinda.

2) Kuwa kuna hasara kubwa inayoweza kujitokeza.

3) Katika mizania, mleta maombi ataumia zaidi kama maombi yatakataliwa kuliko mjibu maombi kama maombi yatakubaliwa.

Nakubaliana na wakili wa mjibu maombi kuwa ni msimamo wa sheria kwamba vigezo hivi ni lazima viwepo vyote kwa pamoja ili kukidhi kuishawishi Mahakama kuruhusu maombi ya zuio la muda.

Tukianza na kigezo cha kwanza, haina ubishi kwamba kuna shauri Tume ya Usuluhishi ambalo linasubiri kuamua mgogoro wa kikazi kati ya wadaawa. Nakubaliana na wakili wa mleta maombi kuwa, hata katika maombi haya kuna ubishi unaojitokeza kuhusiana na kuwepo

kwa shauri katika baraza la usuluhishi. Na pia nakubaliana na mleta maombi kuwa uwepo wa uwezekano wa kushinda si jambo la kuweza kuamuliwa katika hatua hii. Kwa vile ye yote anaweza kushinda katika shauri la tume, ijulikane tu kwamba hata mleta maombi anaweza kushinda. Itoshe tu kusema kuwa kwa vile hakuna ubishi kuwa kuna shauri Tume ya Usuluhishi, basi kigezo cha kwanza kimetimia.

Kuhusu kigezo cha pili cha kuwepo kwa hasara kubwa kwa waleta maombi, ni msimamo wa sheria kuwa hasara hiyo ni lazima iwe ni hasara isiyoweza kufidiwa kwa namna yoyote. Moja ya kesi iliyotoa msimamo huu ni **Kaare vs. General Manager Mara Cooperation Union [1924] Ltd. (1987) TLR 17.**

Nakubaliana na mawasilisho ya mleta maombi kuwa mjibu maombi ni kampuni ya kitanzania, inayomilikiwa na watanzania na inayoendelea na biashara nchini. Jambo hili halijabishaniwa. Sijaona maelezo yanayotosha kutoka kwa waleta maombi kuwa nje ya mali wanazotaka zitolewe zuio la kuuzwa, wajibu maombi hawana uwezo mwingine kifedha au kimali ambao utamwezesha kulipa waleta maombi kama watashinda tuzo. Kwa msingi huu, na kwa vile kampuni na wamiliki wote ni watanzania, naona hakuna maelezo ya kutosha kuonyesha ni kwa jinsi gani waleta maombi watapata hasara isiyoweza kufidiwa kwa fedha au namna nyingine nje ya mali wanazotaka zisiuzwe. Ukazaji wa hukumu una njia nyingi ikiwemo kuwakamata wadeni tuzo, hivyo kwa wadaiwa ambao ni watanzania, sioni sababu ya hofu upande wa waleta maombi.

Kuhusu kigezo cha tatu, ni nani atapata hasara kubwa kati ya waleta maombi kama maombi yatakataliwa au wajibu maombi kama maombi yataruhusiwa, inaonekana kila upande unaweza kupata hasara. Hata hivyo, hakuna mahali wajibu maombi walipotoa maelezo ya kina kuonyesha ni viashiria gani vimewafanya wahisi kuwa mali walizotaja zina mpango wa kuuzwa. Hakuna kielelezo chochote kama tangazo la mauzo au mazungumzo na wanunuzi ambayo yamejitokeza na kuelezewa na waleta maombi kusababisha hofu ya uuzwaji wa mali hizo. Kukosekana kwa maelezo haya kunaiweka Mahakama hii katika hatari ya kuruhusu mali zinazotumika katika kuendesha kampuni kuwa mikononi mwa waleta maombi na kuisababishia kampuni kufilisika jambo ambalo haliwezi kurekebika kirahisi. Mpaka sasa hakuna ushahidi wowote kuonyesha kama kampuni ya mjibu maombi ina mwelekeo wa kufilisika na hivyo kuja kushindwa kulipa deni tuzo kama waleta maombi watastahili kulipwa.

Ikumbukwe pia kwamba, mali zilizokamatwa na waleta maombi, hazina uhusiano wa moja kwa moja na madai yaliyopo katika Tume ya Usuluhishi. Madai ya tume yanahusu fedha, ambazo kulipwa kwake, si lazima kutokane na mauzo ya mali walizoshikilia. Mali hizo hazina mgogoro wa umiliki katika Mahakama yoyote, hivyo sioni sababu ya kumkataza mwenye nazo kuzitumia kwa kadiri atakavyoona inafaa.

Kutokana na uchambuzi huu, hata kigezo cha tatu hakijajitosheleza kuishawishi Mahakama hii kutoa amri ya zuio.

LabourCourt.Tz

Katika hatua hii, nimeona ni vema kuweka wazi kuwa, ingawa maombi ya faragha yalikuwa pia na ombi la kuomba wajibu maombi kulipa SHS 455,298,247. Hata hivyo, wadaawa hawakuliongelea jambo hili katika mawasilisho yao hivyo na mimi sitalizungumzia.

Baada ya kuona kuwa kigezo cha kwanza na cha pili cha maombi hakijajitosheleza, naona waleta maombi hawajaweza kuleta sababu za msingi kuifanya Mahakama itoe amri ya zuio dhidi ya wajibu maombi. Hivyo hoja **kama waleta maombi wameweza kutoa sababu za msingi za kuishawishi Mahakama kuruhusu ombi la zuio la muda** inajibiwa kinyume chake kwamba, wajibu maombi wameshindwa kuishawishi Mahakama kuwa kuna sababu za msingi kuiwezesha kutoa amri ya zuio dhidi ya wajibu maombi.

Kwa sababu zilizoelezwa, Maombi haya yanatupiliwa mbali kwa kukosa msingi. Imeamriwa hivyo.

Imetolewa leo tarehe 06 Julai, 2022, Dar es Salaam.

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA (The High Court of Tanzania) DIVISHENI YA MAHAKAMA YA KAZI (Labour Division)

**KATARINA REVOCATI MTEULE**

**JUDGE**

**06/07/2022**